

# HALMASHAURI YA MANISPAA YA SUMBAWANGA

Simu: 023-2802163

Fax: 025-2802163

E-mail: [md.sumbawanga@rukwa.go.tz](mailto:md.sumbawanga@rukwa.go.tz)

*Unapojibu Tafadhali Taja:*



Mkurugenzi wa Manispaa

S.L.P. 187

SUMBAWANGA

SMC/C.20/11/06/ 93

26/08/2017

## TANGAZO LA KAZI

Mkurugenzi wa Manispaa ya Sumbawanga anawatangazia raia wa Tanzania wenye sifa hitajika, -nafasi NNE(4) za kazi kama zilivyotolewa na Katibu Mkuu OR-UTUMISHI kupitia Kibali cha Ajira Mbadala chenye Kumb.Na. CFC 26/205/01"FF"/91 cha tarehe 22/08/2017.

Namna ya kutuma maombi, Anuani, Sifa na mwisho wa maombi ya kazi imeoneshwa hapo chini:

### **1: NAFASI ZA KAZI: MTENDAJI WA KIJIKI Daraja la III(VEO III) ; Nafasi 4**

#### **E. SIFA ZA MWOMBAJI:**

3. Anatakiwa awe amehitimu kidato cha Nne au Sita(Form IV au VI),
4. Awe amehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo:Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo , Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

**[ANGALIZO: Astashahada /Cheti kiwe na ngazi ya NTA -LEVEL 5]**

#### **F. KAZI NA MAJUKUMU:**

- Afisa masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji,
- Atakuwa Katibu wa vikao vya Serikali ya Kijiji.
- Atakuwa ni mlinzi wa amani katika kijiji/msimamizi wa masuala ya ulinzi na usalama wa raia na mali zao.
- Kusimamia miradi mbalimbali ya maendeleo katika Kijiji
- Mwenyekiti wa kikao cha Wataalamu wote waliomo ndani ya kijiji
- Kusimamia utungaji na utekelezaji wa Sheria ndogo katika Kijiji
- Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na kutunza kumbukumbu mbalimbali za Kijiji.

**G. MSHAHARA:**

- Cheo cha Mtendaji wa Kijiji kiko katika ngazi ya **TGS B**, yaani **Tsh. 390,000/=**kwa mwezi.

**H. UMRI:** Mwombaji awe na umri kati ya miaka 18 na 45

**NAMNA YA KUTUMA MAOMBI:** Maombi yaambatanishwe na nakala ya:-  
1.Cheti cha Taaluma, 2.Cheti cha Ujuzi, 3. CV, 4.Cheti cha Kuzaliwa na Picha(Passport Size) 1; Na maombi yatumwe kwa Posta au kuletwa Masijala kupitia anuani ifuatayo:


**MKURUGENZI WA MANISPAA,  
S.L.P. 187,  
SUMBAWANGA**

**MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI:**

Mwisho wa kutuma na kupokea maombi ni tarehe **08/09/2017** , siku ya Ijumaa saa **09:30 Alasiri** .

**NB: VYETI VYA KUGHUSHI HAVITAKIWI KABISA; UHAKIKI UTAFANYIKA.**

**Tangazo hili limetolewa na:**

  
SAAD MTAMBULE  
KAIMU MKURUGENZI WA MANISPAA  
SUMBAWANGA



**NAKALA: MBAO ZA MATANGAZO (NDANI NA NJE YA MANISPAA )**